



Kusimulia hadithi—ziwe za kweli au za kubuni—ni njia nzuri ya kutangamana na mtoto wako.

Kwa pamoja, mnaweza kukumbuka matukio halisi katika maisha ya familia yako. Kila mtu anaweza kufurahia kusimulia tena hadithi kulingana na anavyoikumbuka. Pia unaweza kushiriki hadithi za ukiwa mtoto au kusimulia tena hadithi za jadili kutoka kwa tamaduni yako ili kusaidia kuelezea masomo muhimu ya maisha na kumpa mtoto wako hisia ya kustahili.

Kusimulia hadithi ni jambo la ajabu. Hadithi humsaidia mtoto wako kuwa mbunifu na kuelewa ulimwengu unaomzunguka. Ni njia nzuri pia ya kuondoa hofu na kumsaidia mtoto wako kuhisi vizuri zaidi na mabadiliko katika maisha yake. Mwishowe, hadithi ni njia nzuri ya kumsaidia mtoto wako kujifunza kuelewa na kuzungumza vyema lugha yake ya nyumbani- na hii itamsaidia kujifunza lugha mpya!

Vidokezo vya Kusimulia Hadithi:

- Tumia lugha safi na rahisi.
- Rudia kile mtoto wako anakisema, ili mtoto wako aone kwamba unaelewa.
- Msaidie mtoto wako kujifunza maneno na fikra mpya.
- Zungumzia kuhusu watu, maeneo na vitu anavyovijua.
- Msaidie mtoto wako kujifunza maneno na fikra mpya.
- Mpe nafasi ya kuzungumzia kuhusu vitu muhimu vya kibinafsi.
- Uliza na ajibu maswali.
- Sikiliza na muongee pamoja kwa lugha yako ya nyumbani.
- Simulia tena na tena hadithi ambazo mtoto wako anazipenda.
- Furahia kusimulia hadithi kwa lugha yako ya nyumbani ikiwezekana.

Kusimulia hadithi huunda ujuzi wa lugha.

Utafiti umeonyesha kwamba kuongea kuhusu matukio, tamaduni na hisia za familia kwa lugha yako ya nyumbani kunaweza kusaidia sana ukuaji wa mapema wa mtoto wako. Tunajua pia kwamba wakati mzuri zaidi wa kukuza ujuzi wa lugha ni wakati mtoto wako ana umri wa miaka sufuri hadi miaka mitatu. Huu ndio wakati ubongo wake uko tayari kuhusisha lugha. Maneno zaidi anayoyasikia watu huu, ndio maneno zaidi ataweza kuyaelewa na kujifunza. Anavyoendelea kujua na kutumia maneno zaidi, ndivyo ana uwezo zaidi wa kuwa msomaji mzuri. Kuweza kusikiliza na kuongea, kwa lugha yoyote, ni ujuzi msingi wa kuwa tayari kuanza shule.

Simulia hadithi kwa lugha yako ya nyumbani.

Kuongea, kusikiliza na kusimulia hadithi kwa lugha yako hutoa msingi thabiti wa kujifunza lugha ya pili. Endelea kutumia lugha yako ya nyumbani na mtoto wako. Itamsaidia kuhisi ameunganishwa zaidi kwako na familia nzima. Atakuwa na uwezo zaidi wa kukua akijivunia lugha na utamaduni wake. Tunajua kwamba msingi thabiti wa lugha yako ya nyumbani utafanya kujifunza lugha ya Kiingereza iwe rahisi kwa mtoto wako.

Inapendekezwa pia kwamba wazazi wasichanganye lugha au kuacha kutumia lugha ya nyumbani. Endelea kuongea, kusimulia hadithi na kuzungumza kwa lugha yako ya nyumbani ili kuiendeleza na kuifanya iwe thabiti. Hii itamsaidia mtoto wako kujifunza lugha ya pili kwa haraka na vizuri zaidi.

Kusimulia hadithi kwa lugha yako ya nyumbani na kuchukua muda wa kusikiliza hadithi za mtoto wako humsaidia kwa njia nyingi:

- Atahisi kuwa ni wa maana, amesikilizwa na amethaminiwa.
- Atahisi karibu na wewe kwa kuwa anatiwa moyo kushiriki mawazo na hisia zake.
- Atavutia zaidi na vitabu.
- Anaweza kujifunza maneno na fikra nyingi kwa lugha yako.
- Anahimizwa kuongea na wewe kwa lugha yako ya nyumbani.
- Mtoto wako atajifunza kukumbuka matukio, kuelezea hadithi, kufanya maamuzi na kuongea kuhusu kila kitu anachokifanya.
- Atajifunza kugundua sauti zilizorudiwa na kujua maneno. (Huu ndio mwanzo wa kujifunza kusoma.)

Fikra ya Shughuli: Tengeneza Kitabu cha hadithi na Mtoto Wako

- Unaweza kutumia michoro au picha za mtoto wako kutengeneza kitabu cha hadithi.
- Ongea na mtoto wako kuhusu michoro yake au kuhusu hadithi ya familia ambayo angependa kuiweka kwenye kitabu.
- Mtie moyo mtoto wako kukuambia maneno ya kutumia kwa hadithi kwa lugha yako ya nyumbani.
- Chapisha maneno hayo kwa lugha yako ya nyumbani.

Tembelea cmascanada.ca/cnc/parents kwa maelezo zaidi ya lugha mbalimbali ya wazazi



SUPPORTING CHILD CARE IN THE SETTLEMENT COMMUNITY / SOUTIEN DE LA GARDE DES ENFANTS DANS LA COMMUNAUTÉ DE RÈGLEMENT
Funded by: Immigration, Refugees and Citizenship Canada / Financé par : Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada